# JARIDA

## LA MSANII

TOLEO LA SITA, OKTOBA 2024

BARAZA LA SANAA LA TAIFA-BASATA
NATIONAL ARTS COUNCIL




**Tuzo za Muziki Tanzania 2023....................**

Dirisha la kuwapigia kura wanamuziki watakaowania Tuzo za muziki Tanzania (TMA) limefunguliwa rasmi tarehe 03 Septemba, 202

**Tuzo za HAPAWARDS Nchini.................**

Lengo la tuzo hizi ni kuendelea kuwajenga wasanii na wadau wa sanaa pamoja na kuwapa fursa ya kujulikana kimataifa,

## YALIYOMO


Utangulizi.......................................................01
Uchongaji.......................................................02
Watengenezaji Maudhui....................................04
META kunufaisha Wasanii.................................05
Tuzo za Muziki Tanzania 2023..........................07
Kutana na Msanii ..............................................10
Tuzo za HAPAWARDS Nchini............................14
Naibu Katibu Mkuu azuru BASATA...................12



**BODI YA UHARIRI:**

**MWENYEKITI**
Dkt. Kedmon Mapana

**MWANDISHI**
Isack Bilali

**USANIFU**
Sehemu ya Sanaa za Ufundi

**PICHA**
Nicholaus Jofrey



Jengo la Utumishi,
8 Barabara ya Kivukoni,
S. L. P 4779, Dar es Salaam,
TANZANIA
Simu: +255 738 259 611/481,
Barua Pepe: km@basata.go.tz
info@basata.go.tz,


**Mfumo wa Wadau wa Sanaa,**
**Jisajili kupitia: https://sanaa.go.tz**

**www.basata.go.tz**

basata.tanzania

## "Uchongaji" hazina ya Sanaa isiyovuma

Wahenga walinena "mvumilivu ula mbivu" usemi unahitajika sana katika kazi ya sanaa ili kuwatia moyo wasanii hususani wa uchongaji ambao wakati mwingine kazi zao uchukua muda mrefu sana kabla ya kuonwa hii inatokana na changamoto lukuki zinazoikabili sekta husika ikiwemo kutoimbwa au kusemwa miongoni mwa wadau wa Sanaa au jamii husika.

Kutokana na sababu hiyo na ukosefu wa ajira miongozni mwa jamii watu wengi wamejikuta wakikumbuka kuendeleza vipaji vyao vya sanaa iwe ya kuimba, kuchora na hata kuchonga vinyago kama alivyo Mzee John Henrick mkazi wa Mbagala kwa Mbiku jijini Dar es salaam ambaye kimsingi aameamua kuichukulia sanaa ya uchongaji kuwa ni ajira na kukidhi mahitaji Pamoja na changamoto kubwa inayohitaji uvumilivu wa hali ya juu kufikia malengo tarajiwa ya msanii.
Sanaa ya uchongaji inafahamika sana nchini huku ikihusishwa moja kwa moja na kabila la wamakonde kutokana na historia ya kazi nyingi za kuchongwa hususani vinyago vilivyojipatia umaarufu imefanywa na kabila hilo, historia inatuweka wazi kuwa vinyago vinavyopatikana kwa wingi zaidi ni vya wanyama, mashetani na ujamaa ambapo katika sanaa ya uchongaji, ujamaa ni vinyago vyenye mkusanyiko au mrundikano wa watu wengi.

Kwa asili Mzee John Henrick alizaliwa miaka zaidi ya 70 iliyopita huko Mkoani Mtwara katika Kijiji cha Mkunya Wilayani Newala akasoma hadi darasa la nne kabla ya kujiunga na Shule ya kati "middle school" huko Ndanda wilayani Masasi Mkoani humo ambako alianza kuvutiwa na utaalamu wa uchongaji uliokuwa unafanywa na Wajerumani wakishirikiana na wakaazi wa huko kwa kutumia mawe hivyo baada ya kumaliza masomo yake alirudi nyumbani Newala ambapo hakukaa muda mrefu kabla ya kuhamia Mtwara mjini ili kuendelea na kibarua Pamoja na kuanza Sanaa ya uchongaji kwa kutumia mti wa mpingo.

Ukimwona mzee huyu ni buheri wa afya. anasema alianza kujishughulisha na uchongaji vinyago akiwa badao mdogo mnamo mwaka 1963 mkoani Mtwara, baada ya kufundishwa na kaka yake aliyeitwa Dihenga ambaye kwa sasa ni marehemu (Mungu amlaze mahali pema).

Kwa kipindi hicho uchongaji haukuwa kama sehemu yake ya msingi katika kujiingizia kipato bali alifanya kama sehemu ya kujifurahisha hadi pale kwa mara ya kwanza miaka ya mwanzoni mwa 1976 alipopata bahati ya kuingia makubaliano na taasisi moja kuwatengenezea vinyago kwa malipo ambayo yaliweza kubadilisha mfumo wa Maisha yake ikiwemo kujenga makazi ya kudumu na kuhamia jijini Dar es salaam ili kujitanua kwenye soko la Sanaa ya uchongaji.

"Nilihamia Dar es Salaam mwaka 1979, nikaweka kituo kule Mkuranga (kwa sasa iko Mkoa wa Pwani) kwa ajili ya kuchonga na kuuza vinyago," anasema Mzee Henrick na kuendelea,



Mzee John Henrick (78) ni fundi wa kuchonga vinyago aliyeaminika na watu wengi ambapo alifanikiwa kushirikiana katika majukumu yake na wasanii wenzake kam vile Marehemu Mzee Livanga, kwa sasa anapatikana mitaa ya mbagala ambako anatumia muda mwingi sana kukaa na familia yake mara baada ya kupumzika shughuli za uchongaji kiushindani kutokana na umri ingawa mara chache sana anafanya kazi kwa makubaliano maalum endapo ikitokea mdau atakaekubaliana nae malipo kwa usahihi.

Anasema wakati wa enzi zake yupo kwenye kilelele cha mafanikio ya uchongaji alikuwa anatumia mtindo wa kuangalia mawingu na kutoa kinyago chenye kupendeza sana, muda kwahiyo yeye ni miongoni mwa wasanii wanaoongozwa na mawingu kubuni uchongaji vinyago vya mashetani.

"Enzi zangu wakati nina nguvu za kutosha, hisia zangu zilininipeleka kuchonga sana mawingu, yaani nlikuwa naangalia mawingu nachonga kinyago cha mashetani," anasema Mzee Henrick.

Mzee Henrick anasisitiza kuwa kazi zake zote amezitengeneza kwa kutumia miti aina ya mpingo na mninga kwaajili ya kuchonga wanyama, watu na vitu vingine mbalimbali hivyo yeye na wengine walikuwa wananunua miti hiyo kwa wachuuzi wanaoisafirisha kutoka mikoa ya Pwani na Tanga.

Kwa sasa kazi hii imekuwa na changamoto kubwa sana kutokana na maendeleo ya teknlojia na soko kutanuka hali inayosababisha watu wachache kutawala sanaa husika hata kama hawana vipaji bali wanaongozwa na uwezo wao kiuchumi hivyo kuteka mfumo mzima wa uendeshaji wa sanaa ya uchongaji.

"Niliamua kujikita katika uchongaji unisaidie kimaisha lakini kwa sasa kazi hii naiona ngumu, imevamiwa zaidi na watu wenye uwezo mkubwa kiuchumi ambao kimsingi hawana utaalamu wa uchongaji."

Anasema kuwa, wenye uwezo wanachukua mafundi wanaowatengenezea vinyago majumbani kwao kwa ajili ya kuviuza kwenye maduka yao hapa nchini na kusafirisha vingine kwenda kuviuza nje yan chi hususani nchi za Ulaya, Amerika na kwingineko anasisitiza kuwa hao ndiyo wanaofifisha sanaa hii, unakuta wachongaji hawapati wateja sahihi ila asiye msanii anapata fursa ilhali msanii mwenyewe hazipati.

Kitu kingine kinachosababisha sanaa hiyo kusahaulika ni aina ya wateja waliotawala soko lao ambapo kimsingi wateja wakuu wa vinyago wanavyochonga ni wageni hususani wazungu kutoka mataifa tofauti yaliyopo bara la Amerika, Ulaya na Asia.

Kwa mujibu wa mzee huyu, Waafrika wanaojitokeza zaidi kununua vinyago katika kituo chake cha kazi, walikuwa ni Waganda, Wazambia na Waafrika Kusini, ingawa haikuwa mara kwa mara na miezi iliyokuwa inalipa zaidi ni msimu wa Julai hadi Disemba ndiyo msimu mzuri unaochangamsha biashara katika mauzo.

"kiukweli kuanzia mwezi Julai hadi Disemba ndiyo kidogo biashara inakuwa imechangamka, lakini miezi mingine ndiyo sanaa inakuwa ya njaa kwa sana," anasema huku akiendelea kupiga msasa kinyago cha ujamaa.

Kutokana na ushuhuda wa wachongaji na wauzaji wa vinyago hapa nchini, wateja wengi wanapendelea kununua vinyago vya wanyama, hasa tembo, faru, nyati, twiga na simba, ambapo Waingereza na Wachina ndiyo wanaopendelea vinyago vya wanyama, huku Wamarekani na Wajerumani wao wanapendelea vinyago vya mashetani.

"Ukifuatilia taarifa ya soko utagundua kuwa Wamarekani na Wajerumani wanapenda sana vinyago vya mashetani huku Waingereza ndiyo hawataki kabisa mashetani," anasisitiza mchongaji huyu.

Mzee John Henrick anasema bei ya kwanza ambayo ni kubwa kabisa aliyouza kinyago ni Tzs 700,000 ambayo aliwahi kuuza miaka ya mwanzoni mwa 1990 anakumbuka ilibadiliMaishaa yake kwa kiasi kikubwa sana ingawa haikuwa ya kinyago kimoja ilikuwa ni mjumuiko wa kazi nyingi zilizochukuliwa kwa wakati mmoja na wateja kutoka Marekani.

Amekiri kuwa kwa sasa mfumo wa uendeshaji sanaa ya uchongaji imesababisha ukosefu wa soko la uhakika hivyo kuwa kikwazo kikuu kinachodumaza uchumi wa wachongaji na wauzaji wa vinyago nchini ingawa kuna nguvu kubwa kutoka serikalini inatumika kuirejesha tasnia kwenye mstari wake lakini wadau wake wanatakiwa kuitafsiri kwa vitendo.

"Ingawa hatuna soko la uhakika, Serikali imetjitahidi kufungua fursa kwa wadau wa sanaa zote ikiwemo uchongaji, na viongozi wanatembelea maeneo mbalimbali yenye shughuli za sanaa, kwa sasa watu wanakopeshwa hivyo ni muda sahihi kutafsiri juhudi za serikali kwa vitendo," ameongeza Henrick.

Mzee Henrick inampa ujasiri wa kujitokeza mbele ya jamii kutoa ushuhuda wa hazina ya sanaa hii ambayo kwa sasa imefifia sana, anaweka wazi kuwa sanaa yake si haba imeweza kumpatia mafanikio kidogo yanayomwezesha kujigharamia Maisha yake na ujenzi wa nyumba ya kuishi eneo la Mbagala, Dar es Salaam, hayo yote yametokana na kipato cha uchongaji vinyago.

Imepita zaidi ya miaka 50 sasa tangu Mzee Henrick aanze kujishughulisha na uchongaji na uuzaji vinyago, lakini amepata nafasi ya kushiriki mara tatu katika maonesho ya biashara nje ya Tanzania.

"katika miaka yangu takribani 50 ya uchongaji nimewahi kuhudhuria maonesho matatu ya biashara nje ya Tanzania, ambayo yalifanyika katika nchi za China, Canada ba Afrika ya Kusini, kilichomichanganya baadhi ya wengi niliohudhuria nao si wachongaji bali wenye uwezo kifedha na wanufaika haswa wa sekta hiyo huku wasanii wakiachwa" anasisitiza.

Anashukuru kwa sasa kuna mwanga unaonekana katika tasnia ya uchongaji mara baada ya serikali kutoa fursa ya mikopo, kwahiyo yeye kama msanii pamoja na umri kumtupa anawasihi wasanii wachanga kuchangamkia fursa iliyopo mbele yao kwakuwa hii ilikuwa kilio chao cha muda mrefu sana juu ya mitaji, imechukua muda mrefu sana kupata majibu haya ya uwezeshaji kutoka Serikalini wenye lengo la kuwatafutia masoko ya uhakika na kuwakopesha fedha za mitaji wajikwamue kiuchumi na kuboresha maisha yao na familia zao.

Anatumia nafasi hii pia kuieleza jamii kwamba wachongaji wanaweza kujikwamua kiuchumi, ikiwa watu watajenga mazoea ya kununua bidhaa za uchongaji kutoka kwa wachongaji husika kuliko kwa wachuuzi wanaonufaika na kazi wasizozitolea jasho.

Kuna muda kazi inakuwa ngumu sana unapokutana na mteja wa kigeni alafu msingi wa mawasiliano yenu inakuwa lugha yaani watu kama Wachina ambao wengi hawajui Kiswahili na hata Kiingereza hawakiwezi sana. hivyo inakupasa kuwa mjanja katika kufanya nae biashara na kwa enzi hizo ilikuwa wanaongea kwa vitendo tu huku nyenzo kuu ikiwa kikokotoo lakini kwa sasa kwenye ulimwengu wa teknolojia kila kitu kinamalizwa na simu janja.

"Ni kweli zamani ilikuwa shughuli kwenye kukubaliana biashara, ilitulazimu kutumia calculator kuwasiliana nao kuhusu bei ya bidhaa wanayohitaji, unamwandikia bei ya kuanzia nae anakuandikia kiasi alichonacho, hadi nakubaliana, jambo hili kwa sasa linamalizwa kiurahisi na simu janja" ameweka wazi Mzee Henrick.

Anakiri kuwa sanaa hii ni hazina kweli, anakumbuka zamani sana Serikali iliwaondoa kandokando ya barabara za Bagamoyo na Oysterbay ikawahamishia kituo cha Mwenge miaka ya 1983 wengine wakatawanyika kwenye maeneo yao binafsi akiwemo yeye mwenyewe wakati huo idadi yao haikuwa kubwa sana.

Kwa sasa serikali inafanya nao kazi bega kwa bega kupitia Chama cha Wasanii Wachongaji Tanzania (CHAWASAWATA) kikisimamiwa na Shirikisho la Sanaa za Ufundi (TAFCA) ambapo muunganiko wake unaleta ushirikiano madhubuti wa kiutekelezaji majukumu kufikia BASATA na mwishowe Wizarani ambapo mara nyingi wameweza kupata mafunzo na mambo yao kusikilizwa kisha kupatiwa ufumbuzi kwa wakati.

Serikali na wadau wa sanaa wameonesha kutambua kuwa uchongaji ni sanaa muhimu katika kutangaza utamaduni wa Mtanzania, na kwamba bila wachongaji utamaduni wa taifa letu unaweza kutoweka.

Kihistoria na nadharia nyingi zinawataja Wamakonde na Wazaramo kuwa ndio waasisi wa sanaa ya uchongaji, lakini kwa siku za hivi karibuni makabila yote zaidi ya 120 hapa nchini yana watu wenye vipaji vya kuchonga vinyago kiasi kwamba sanaa hiyo imeonesha kuenea kwa kasi hivyo kuwa kielelezo cha utamaduni.

"Kitu kingine, kama kweli Serikali inataka kuona sanaa ya uchongaji inasonga mbele, iweke mkakati wa kusaidia kumotisha wasanii husika ili nao wasaidie kuweka hai utamaduni wa taifa letu," anaongeza Mwenyekiti huyu.

Ameendelea kuwasihi viongozi wa Serikali kutambua kuwa ofisi zao nazo ni sehemu ya soko la kutangaza bidhaa za uchongaji, litakalowezesha wasanii husika kupiga hatua ya maendeleo hivyo wana budi kununua bidha hizo kwa wingi na kufanya mapambo katika ofisi zao ili wageni mbalimbali watakapokuja iwe chanzo cha kuwatangazia bidhaa.

Anaikumbusha jamii ya Watanzania na Waafrika kwa jumla kuchangamkia bidhaa za uchongaji badala ya kuendelea kuamini kimakosa kuwa bidhaa hizo ni kwa ajili ya mapambo kwenye ofisi na nyumba za raia wa kigeni pekee.

Katika kumalizia Mzee Henrick, amewahasa wasanii mbalimbali hasa wa sasa hivi kutumia muda mwingi kujifunza mambo mbalimbali ili yawaongezee ujuzi na ubunifu wa kazi zao ziweze kuwa bora Zaidi ya zile za kipindi chao kwakuwa uwezo wa kuliteka soko la kitaifa na kimataifa upo kama wakiamua kushikamana na kufanya kazi kwa bidi, anaamini muda si mrefu "Uchongaji utakuwa Sanaa inayovuma".

## Watengeneza maudhui kuanza kupata maokoto

Mkurugenzi Mkuu wa tume ya tehama (ICTC) Dkt Nkundwe Mwasaga amevitaka vyombo vya habari nchini na watenegeza maudhui mitandaoni kutumia vema fursa ambayo inakuja ili kutengeneza maudhui mazuri ya Kiswahili yatakayo-chechemua uchumi wa kidijitali na kukuza kipato.

Ameyasema hayo tarehe 15 Agosti, 2024 katika ukumbi wa maktaba mpya ya chou kikuu cha Dar es salaam wakati wa hotuba ya ufunguzi wa mafunzo ya ulipwaji watenegeneza maudhui ya mitandao ya kijamii ya kampuni ya meta.

"Siku ya leo ni muhimu sana kwa wasanii wetu, wana habari na watengeneza maudhui, tunaona namna zile 4R zinavyofanya kazi hasa upande wa mageuzi yaani Reforms...haya sasa ndo mageuzi ya kiuchumi kwenye tasnia ya ubunifu ambayo ni matunda ya serikali ya awamu ya sita" alibainisha Dkt Nkunde.

Mafunzo hayo yameandaliwa kwa ushirikiano wa Baraza la Sanaa la taifa, shirika la umoja wa mataifa la elimu, sayansi na utamaduni (UNESCO) na kampuni ya META yakihamasishwa na ujumbe wa "fahamu fursa za kidijitali kwa maendeleo endelevu"

Kutokana na mabadiliko makubwa yanayoendelea kufanyika katika kiwanda cha ubunifu kupitia teknolojia leo hii wadau wanashuhudia jambo la msingi kabisa kupata kutokea ambalo litawanufaisha katika kazio zao, mitandao ya kijamii siyo sehemu ya kuwasiliana tu bali ni chanzo cha mapato halali katika kazi zao.

Mkurugenzi Buganga amesisitiza kuwa kwa kipindi kirefu wasanii wametumia mitandao ya kijamii kufikisha maudhui kwa mashabiki wao Pamoja na kufikisha jumbe mbalimbali za serikali kwa wanajamii juu ya ushirikishwaji wa masuala mbalmbali na leo hii inaongeza thamani yake kuwa sehemu ya kuingiza kipato kwa jamii hayo ndiyo manufaa ya maendeleo.

Kwa takwimu zilizotufikia ni kwamba mitandao ya META ina watumiaji Zaidi ya bilioni 3.5 duniani kote hivyo kama watumiaji hao wote wangengekuwa nchi ingekuwa inaongoza kwa kuwa na wananchi wengi kwahiyo ni mtaji wa kutosha sana kuweza kujiongezea kipato iwapo msanii atazingatia kupandisha maudhui yenye tija na kukonga nyoyo za wanaomfuatilia bila kuathiri taratibu zinazoongoza matumizi ya mitandao.

Ameendelea kusema kuwa huu ni muda muafaka kwa waasanii na wadau wa Sanaa kujiongezea ujuzi ili waweze kuutumia katika kuandaa na kupandisha maudhuo yenye kuzingatia maadili katika kurasa zao, amewaasa kutotumia fursa vibaya bali iwe chachu ya kufanya kazi kwa bidi na maarifa ya hali ya juu kwa manufaa yao na kizazi kijacho.

Sanjari nae mkuu wa ofisi ya UNESCO Dar es salaam Michael Toto ameishukuru sana serikali kupitia BASATA kwa ushirikiano waliotoa pamoja na kuwataka wasanii na wadau wa Sanaa kuchangamkia fursa hiyo kwa kadiri kasi ya maendeleo ya teknolojia yanvyotaka pia amesisitiza kuendelea kutoa elimu kwa kadiri itakavyobidi kwa ushirikiano na BASATA na META.




unesco Meta

## Watumiaji Bilioni 3 META kunufaisha "Content Creators" Tanzania

Mwakilishi Mkazi wa UNESCO Tanzania, Bw. Michael Toto, amesisitiza umuhimu wa matumizi sahihi ya mitandao kwa watengeneza maudhui watakaonufaika na mapato kutoka kwa watumiaji zaidi ya bilioni tatu wa mitandao ya META duniani kote huku akiahidi shirika lake litakuwa mstari wa mbele kuhakikisha linatoa elimu ya kutosha juu ya matumizi sahihi ya mtandao.

Ameongea hayo wakati wa mafunzo ya namna ya kupata malipo kwa watengeneza maudhui, wadau wa sanaa na wasanii wanaotumia mitandao ya META yaani "Facebook, Instagram na Whatsap" ambao wameanza kupata malipo kulingana na kukidhi vigezo na masharati yaliyowekwa na kampuni hiyo.
"Watumiaji wa META kwa sasa wapo zaidi ya bilioni tatu na kama ingekuwa ni nchi basi ingekuwa na watu wengi kuliko nchi yoyote, hivyo ni muda muafaka kwa Content Creators wote kujua wanaenda kunufaika na kundi kubwa la watu" amesema Toto.

Aidha, mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Nkundwe Mwasaga, alivikumbusha vyombo vya habari na watumiaji wa mitandao kuongeza umakini na kufanyia uchunguzi maudhui ya mitandaoni kabla ya kuzifanyia kazi kwa sababu ndani yake zipo za kweli na zenye lengo la kupotosha umma.

Amepongeza Shirika la UNESCO, BASATA na META kwa kutoa mafunzo hayo ambayo yataongeza tija katika matumizi ya mitandao kutoka kuwa chanzo cha habari na kuwa chanzo cha kuongeza kipato na Tanzania ni miongoni mwa nchi ambayo ina takwimu nzuri ya watumiaji wa mitandao, huu ni muda muafaka.

Matumizi ya mitandao katika kutoa taarifa yamekuwa kwa kasi sana nchini Tanzania kuanzia mtu mmoja mmoja hadi Taasisi za umma na binafsi, na kwa taarifa njema kabisa hata kwa viongozi wetu wa juu wa serikali wako vizuri katika utoaji wa taarifa kwenye kurasa zao wakiongozwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye nae katika mtandao wa Instagram anaongoza miongooni mwa viongozi wa kisiasa Afrika.

Watengeza maudhui walioanza kujipatia kipato kupitia kampuni ya META ni wale wa Facebook kisha itafuata mitandao ya Instagram na whatsap kwa siku za usoni ambayo nayo ina watumiaji wengi hapa nchini.

Kwa upande mwingine wadau wa sanaa wamewekwa wazi kuwa huu ni muda muafaka kwao kuhakikisha wanaeneza lugha ya Kiswahili kwakuwa maudhui ya lugha ya Kiswahili yanahitajika kutokana na soko lake kwa sasa kuwa kubwa duniani kote.

Pia wataalamu kutoka UNESCO waligusia kuhusu mradi mkubwa uliopo wa kufundisha uchumi wa kidijitali ambao utatolewa kwa viongozi wote wa serikali kisha kuwafikia wananchi kwa ukubwa wao lengo likiwa kutanua fursa na vipato.
Kwa kuongezea, Mkurugenzi wa ukuzaji na Maendeleo ya Sanaa Baraza la Sanaa la Taifa, Bw. Edward Buganga, amemshukuru Rais Dkt Samia kwa kufungua milango ya dipmlomasia ya kiuchumi katika sekta ya sanaa hivyo kupata fursa mbalimbali zinazowanufaisha wadau wake.

Amewasisitizia watengeneza maudhui yenye ubunifu kwa kuzingatia maadili ya Kitanzania pamoja na kujirasimisha kwenye mfumo wa AMIS kupitia kiungo "sanaa.go.tz" mfumo huo unarahisha utoaji huduma kwa wasanii na wadau wa sanaa hususan huduma za usajili na utoaji vibali vya kuendesha shughuli za sanaa nchini.

Baadhi ya watengeneza maudhui kwa nji ya mtandaoni, wakiongozwa na Theresia Nyoni, walisema kupitia mkutano huo wamejifunza mambo mengi hususani elimu kuhusu fursa zinazopatikana mtandaoni na kuomba serikali iendelee kutoa mafunzo kama hayo ili badala ya watu kuitumia vinginevyo iweze kuwanufaisha kiuchumi.



## Wadau wa sanaa watakiwa kufanya haya kupata Maokoto "META"

Meneja wa sera za umma META, Bw. Desmond Mushi, amewataka wasanii na wadau wa sanaa kuzingatia vigezo na masharti ya kuendesha akaunti zao ili waweze kupata mapato kupitia maudhui watakayopandisha kwenye kurasa zao aliyasema hayo jijini Dar es Salaam katika warsha ya kuongeza ujuzi na uelewa unaojumuisha ujuzi sekta ya habari na majukwaa ya kidijitali nchini Tanzania.

Warsha hiyo imeandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na serikali kupitia BASATA, Idara ya Habari (MAELEZO) pamoja na META.
Washiriki waliolengwa ni watengeneza maudhui mitandaoni wakiwemo wasanii, wadau wa sanaa, waandishi wa habari, wanafunzi wa ngazi mbalimbali za elimu, wafanyabiashara na wadau wanaotumia majukwaa ya kidijitali kupandisha maudhui ili kujipatia kipato.

Mushi alisema kwa sasa wameanza na mtandao wa Facebook kwa ajili ya kujifunza na ili watu waweze kulipwa ni lazima maudhui yawe ya mtu husika hivyo kuna kuna wanaofuatilia kuhakikisha uhalali huo.
"Tunachukua muda kuanza na Facebook ili tujifunze halafu itakuja Instagram. Watu watalipwa kwa njia nne, ya kwanza utalipwa kutokana na unachokiweka wewe na matangazo ambayo META inaweka kwenye maudhui yako.

Suala la matangazo ya kampuni ni mtambuka ili kusaidia kuongezeka kwa mapato yanayotumika kuwalipa watengeneza maudhui wa mitandao husika mfano nzuri ni baadhi ya watengeneza maudhui wanaolipwa na mitandao mingine kama You tube.
"Mfano ukiangalia mtandao wa Youtube ukianza kuangalia unakuta kuna tangazo, kwa sababu Youtube anapata fedha inawalipa," alisema.
Mushi alitaja njia ya pili ni "subscription" akimaanisha kwa watakaolipwa ni kupitia mfumo wa kibiashara ambapo watu watatakiwa kujiunga na akaunti ya mtengeneza maudhui kwa kulipia ada itakayomruhusu kuweza kutazama kilichowekwa katika ukurasa wa mhusika.
Njia ya tatu itakuwa ni ya kununua nyota kwenye ukurasa wa mhusika na hivyo fedha zinakuja kwa anayehusika.

Mushi ameongeza kuwa njia ya nne ni ile ambayo inahusisha kampuni kutumia maudhui ya mtu binafsi aliyoweka kwenye ukurasa wake kama wa mtandao wa Facebook na Instagram.

Mushi anaweka wazi kuwa serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alianza mchakato wa kuomba jambo hili tangu mwezi Disemba, mwaka 2021, hayo yote yalikuwa maono ya serikali kwa wananchi wake kulingana na maendeleo ya teknolojia.
Mushi alisema kwa sasa kuna mambo ya msingi ambayo lazima yafanyike ikiwemo kufungua bidhaa na lazima mtu awe na wafuatiliaji "followers" zaidi ya 5,000 ndipo aende kuomba na kuanza kulipwa.

Alisema kigezo kingine kinachoangaliwa ni namna mtu amepata akaunti husika ili kuepuka upatikanaji kwa njia batili kwa sababu baadhi ununua zenye maudhui yanayoshadidia maudhui yenye mmomonyoko wa maadili ambapo wafuatiliaji wake walivutiwa na kuangalia picha au video chafu ndipo wakafika hao 5,000.

Jambo la muhimu linaloangaliwa ni akaunti inafanya kitu gani jambo la malipo lilikuwapo na kuna baadhi ya wasanii watanzania tayari wanalipwa ambao walioanzisha kampuni au akaunti zao zilifunguliwa nchi ya Afrika Kusini na Dubai ila sasa hivi ukiweka akaunti ya Tanzania utalipwa, lakini zamani ilikuwa huwezi kulipwa.
Mwisho kabisa amewapongeza watumiaji wa mtandao wa instagram kwakuwa Tanzania inaongoza kwa kuwa ni nchi yenye watumiaji wenye wafuatiliaji 'followers' kwa nchi za Afrika.




Meta

## Hawa hapa wanaowania tuzo za TMA2023

Dirisha la kuwapigia kura wanamuziki watakaowania Tuzo za muziki Tanzania (TMA) limefunguliwa rasmi tarehe 03 Septemba, 2024 saa 5 usiku mara baada ya kamati inayoratibu TMA chini ya uenyekiti wa David Minja na Makamu mwenyekiti Seven Mosha kuweka wazi vipengele vyote vinavyoshindaniwa na wasanii mbalimbali.

Kipengele cha mwanamuziki bora wa kiume wa mwaka wanaowania ni Marioo wimbo wa "Shisha", Diamond "Shuu", Harmonize "Single again", Ali Kiba "Sumu" na mwisho ni Jay Melody na wimbo wake wa "Nitasema".

Aidha, Kipengele cha mwanamuxziki bora wa kike wa mwaka wanaowania ni Zuchu "Honey", Anjela "Blessing", Malkia Leyla Rashid "wat una viatu" na Nandy "Falling".

Kwa upande wa Bongo fleva mwimbaji bora wa kiume wa mwaka kinashindaniwa na Diamond "Yatapita", Jay Melody "Sawa", Alikiba "Mahaba", Marioo "Love Song" na Harmonize "Single again".

Mwimbaji bora wa kike wa bongo fleva wa mwaka ni Zuchu "Naringa", Appy "Watu feki", Nandy "Falling", Phina "Sisi ni wale" na Anjela "Blessing".

Kwa upande wa wimbo bora wa ushirikiano wa mwaka wanaochuana katika kipengele hiki bni Alikiba ft. Marioo "Sumu", Mboso ft. Chley "Sele", Abigail Chams ft. Marioo "Nani", Jux ft. Diamond "Enjoy" na Diamond ft. Koffi Olomide "Achii".

Katika kipengele cha Albamu bora yam waka walioingia katika mchuano ni Abigail Chams "5", D Voice "Swahili Kid", Navy Kenzo "Most People Want this", Harmonize "Visit Bongo" na Ray Vanny "Flowers III".

Mwanamuziki bora chipukizi wa mwaka wanaoshindania nafasi hiyo ni Pamoja na Xouh "Lalala", Chino Kid "Gibela", Appy "Watu feki", Mocco Genius "Mi Nawe" na Yammi "Namchukia".

Mtifuano wa ngumu kumeza katika wimbo bora wa HipHop wa mwaka unapigwa vikali na wasanii kama Rapcha "Uongo", Country Wizzy "Current situation", Young Lunya "Stupid", Stamina ft Bushoke "Machozi" na Joh Makini "Bobea".

Mwimbaji bora wa Hip Hop ni Young Lunya "Stupid", Kontawa "Dunga mawe", Stamina "Machozi", Joh Makini "Bobea" na Rosa Ree "Mama Omollo".

Huku Mtozi bora wa muziki wa Hip hop wa mwaka wanaowania kipengele hicho ni Black Beatsa "Warrior", S2Kizzy "Maokoto", Ommydaddy "Wanangu kibao", Ringle beatz "Tribulation" na Dupy Beatz "Mr. Christmas part 5".

Kipengele cha Dj bora wa mwaka katika tuzo za TMA kinashindaniwa na Dj D Ommy, Dj Seven Worldwide, Dj Shana Mnyamwezi, Dj Hijab na Dj Mamie. Upande wa utumbuizaji bora wa kike wa mwaka waliotajwa ni Zuchu "Nani remix", Phina "Do Salale", Abigail Chams "Milele" na Da Princess "Lolo".

Mtumbuizaji bora wa kiume wa mwaka kipengele hiki kinawaniwa na Mboso "Sele", Christian Bela "Tamu", Harmonize "Single again", Alikiba "Sumu" na Diamond "Shu".

Mtunzi bora wa muziki wa dansi wa mwaka inawaniwa na wanamuziki wafuatao Master Keys, Dad One Touch, Erast o Mashine, na Christian Bela. Juu ya hapo mwandishi bora wa mwaka waliowekwa katika ushindani ni Pamoja na Mbosso, Dulla Makabila, Thabit Abdul, Jay Melody na Marioo.

Mtozi bora wa muziki wa bongo fleva wa mwaka wanaoshindanishwa ni Ibrah Jacko, Aloneym, Trone, S2Kizzy, na Mr. L huku wanaowania tuzo ya Mtozi bora wa muziki wa mwaka wakiwemo S2Kizzy, Mr. LG, Laizer, Thabit Abdul na Trone.




Mwongozaji bora w avideo wa mwaka ni Hanscana "Maokoto", Nicklass "Dungamawe", Ivan "Sele", Folex "Achii" na Director Wayan "Huku".

Mwanamuziki bora wa mwaka wa nyimbo za asili wanaowania ni Elizabeth Malinganya "Boda boda", Erica Lulakwa "Aragoba", Sinaubi Zawose "Peasa", Ngapi group "berita" na Wamwiduka band "Usizime Muziki".

Wanaowania wimbo bora wa mwaka wa asili ni Sinaubi Zawose "Peasa", Man Fongo na Nyati group "Sauti ya Kumoyo", Erica Lulakwa "Aragoba", Wazawa music band "Muziki hauna mwenyewe" na Wamwiduka band "Usizime Muziki".

Mwimbaji bora wa muziki wa dansi wa mwaka ni Christian Bella "Kanivuruga", Melody Mbassa "Hellena", Papi Kocha "Jela ya Mapenzi", Charlz Baba "Mmbeya" na Sarah Masauti "Popo".

Wimbo bora wa dansi wa mwaka wanaowania ni Diamond ft Koffie olomide "Achii", Melody Mbassa "Nyoka", Malaika Band "Kanivuruga" na Twanga pepeta "Mmbea".

Kwenye upande wa mwanamuziki bora wa dancehall wa mwaka wanaowania nafasi hiyo ni Pamoja na Dj Davizo "Dance hall", Badest 47 "Zagamua", Appy "Mr Hatter"na Bayo the great "Nakupenda". Upande wa wimbo bora wa Dance hall wa mwaka unashindaniwa na Planner "You", Dj Davizo "Dance hall", Badest 47 "Zagamua", Appy "Mr Hatter"na Bayo the great "Nakupenda".

Sanjari na vipengele vilivyotajwa hapo mwanzo pia kuna kipengele cha mwanamuziki bora wa Reggae wa mwaka ambacho kinawaniwa na Akilimali "Africa Mama", Dipper rato "Grateful", Dimateo zion "Rhymes tonight", Ras Nono "Andika" na Warrior from the East "Wewe".

Wimbo bora wa reggae wa mwaka wanaowania ni Warriors from the East "Wewe", Akilimali "Africa Mama", Dimateo zion "Rhymes tonight", Mr Kamanzi "Give and Thanks" na Paul Mihambo "Salamu zako".

Kwa upande wa taarab vipo vipengele vitatu ambavyo ni Mtunzi bora wanaowania ni Father Mauji "umenibamba", Bob Rama "Nkurumbi", Babu Juha "Kisaka", Thabit Abdul "DSM Sweetheart" na Mfalme Mzee Yusufu "Sina Wema"

Huku, Mwimbaji bora wa mwaka inawaniwa na Salha "DSM Sweetheart", Mwinyimkuu "Bila yeye sijiwezi", Malkia Leyla Rashid "Watu na Viatu", Amina Kidevu "Hatuachani" na Mwansiti Mbwana "Sina wema".

Wimbo bora wa taarab wa mwaka unawaniwa ni Malkia Leyla Rashid "Watu na Viatu", Salha "DSM Sweetheart", Mwansiti Mbwana "Sina wema", Mwinyimkuu "Bila yeye sijiwezi" na Amina Kidevu "Hatuachani".

Tuzo nyingine inaenda katika kipengele cha Mtanzania anayeipeperusha vema bendera ya Tanzania Kimataifa (Tanzania Global Icon Award) wanaowania Tuzo hii ni Pamoja na Mchezaji mpira wa miguu Mbwana Samatta, Mwanamitindo Flaviana Matata, Wanasarakasi Ramadhan Brothers Pamoja na Anisa Mpungwe na Clara Luvanda.

Kipengele cha video bora ya muziki yam waka inashindaniwa na Billnass "Maokoto", Mbosso "Sele", Zuchu ft Innos B "Nani remix", Diamond ft Koffie Olomide "Achii" na Harmonize "Single Again".

Turufu ya wimbo bora wa mwaka inachezwa na wasanii wafuatao Zuchu "Honey", Harmonize "Single Again", Jux ft Diamond "Enjoy", Lavalava "Tajiri" na Diamond "Shu".

Kamati hiyo imetaja kipengele cha mwisho kuwa ni "Best song East west and southern Africa" wanaowania ni Libiana "People", Qing Madi "American Love", Asake "Lonely at the top", David ft Musa Keys "Unavailable" na Tyler ICU and Tumelo ft Dj Maphorisa "Mnike".

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mwenyekiti wa kamati hiyo imeweka wazi kuwa upigaji kura utafikia tamati tarehe 28 Septemba, 2024 hivyo wadau wa sanaa waendelee kuwapigia kura wanamuziki katika vipengele walivyotokea kushindania huku usiku wa tuzo za muziki Tanzania ukitarajiwa kufanyika tarehe 29 Septemba, 2024.



# Wananchi wafurika “BASATA” ikikonga nyoyo Kisarawe

Maelfu ya wananchi wilayani kisarawe mkoani Pwani wamejitokeza kwa wingi mitaani kushiriki tukio kabambe la kuibua vipaji vilivyo nje ya mfumo rasmi katika sekta ya Sanaa nchini kupitia programu ya Sanaa mtaa kwa mtaa iliyofanyika tarehe 30 na 31 Agosti, 2024.
Programu hiyo ya siku mbili imeratibiwa na BASATA kwa ushirikiano wa ofisi ya mkuu wa wilaya na Mkurugezni wa halmashauri ya Kisarawe ambapo kwa siku ya kwanza ilihusisha utoaji wa mafunzo ya sanaa katika shule ya sekondari “Sisters of Mary” na Shule ya msingi Kauzeni huku Bwana Oden Manyaga afisa sanaa sehemu ya muziki akijikita kufundisha wanafunzi namna ya kuimba kwa usahihi wimbo wa Taifa na uzalendo.



Juu ya hapo wanafunzi hao kwa nyakati tofauti walipata fursa ya kujifunza namna bora ya uchoraji na kupaka rangi picha mbalimbali kulingana na ubunifu wao, zoezi lilisimamiwa na afisa sanaa sehemu ya ufundi Bi. Jenifa Tarimo ambaye aliwaongoza wanafunzi kuweza kutambua rangi za msingi katika kupendezesha picha Pamoja na mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wachoraji kuhamisha picha zilizo katika ubongo na kuziweka katika mchoro halisi unaoweza kupendwa na watazamaji.

Ratiba ya siku ya kwanza ilihitimishwa kwa mafunzo maalum yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa halmashauri ambapo wasanii na wadau wa sanaa zaidi ya 55 kutoka maeneo mbalimbali wilayani humo kujitokeza na kupata elimu ya kutosha juu ya faida za kujisajili BASATA, uzingatiaji maadili katika sanaa na fursa za masoko katika sanaa yaliyotolewa na Agostino Makame na Abel Ndaga ambao ni maafisa sanaa waandamizi Baraza la Sanaa la Taifa.

Kwa mujibu wa mahudhurio ya mafunzo yote jumla ya wanafunzi 1350 na wadau wa sanaa 55 wamefanikiwa kupata mafunzo ya sanaa na kutambua Baraza na shughuli zake hivyo kujenga msingi mpana miongoni mwao kuwa mabalozi wazuri kwa maendeleo ya sekta ya sanaa hususani katika kutengeneza ajira na kipato.
Programu hiyo iliendelea siku ya pili ambapo maafisa kutoka BASATA wakishirikiana na halmashauri na ofisi ya Mkuu wa Wilaya walifanya matukio ya sanaa mtaani katika vituo vine ambapo walikuwa wanaweka kituo sehemu moja kisha kushirikisha wananchi kuonesha vipaji vyao vya muziki, kuchora, ubunifu na kucheza.



Kukamilisha matukio ya siku ya pili, wananchi walipata fursa ya kushuhudia vipaji vya wasanii mbalimbali waliofanya utumbuizaji katika jukwaaa la pamoja lililoitwa “Vibe la Kisarawe” ambapo kulikuwa na wasanii chipukizi wa Kisarawe pamoja na wanamuziki kutoka Dar es salaam na maeneo mengine nchini wenye hadhi ya kitaifa.
Pamoja na uwepo wa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Mhe Petro Magoti tukio hilo adhimu lilihudhuriwa na mbunge wa jimbo hilo na Waziri wa Viwanda na biashara Mhe. Dkt Suleiman Jafo ambaye alikuwa Mgeni rasmi katika usiku huo na kufurahia shamrashamra za wananchi wake kwa ushirikiano na BASATA.
Katika tamasha hilo wasanii maarufu kama Mzee Yusufu, Siza Mazongeza waliweza kukonga nyoyo za mashabiki wao kwa nyimbo zenye kuamsha furaha na nderemo kwa maelfu ya watu waliohudhuria usiku wa huo wa kipekee uliogubikwa na burudani ya kukata na shoka.
Pamoja na mambo mengine wananchi walifanikiwa kupata ujumbe wa viongozi mbalimbali na watoa hamasa juu ya ushiriki wao katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi novemba mwaka huu utakaofanikisha kuweka madarakani wenyeviti wa vitongoji, vijiji au mitaa Tanzania, kuhakikisha hilo linafanikiwa programu hiyo iliambatana na ujumbe usemao “Sanaa Mtaa kwa mtaa, Shirikishi Uchaguzi wa Serikali za Mitaa”.
Akiongea kwa niaba ya wananchi wa Kisarawe Mhe Mkuu wa Wilaya hiyo Petro Magoti amewashukuru BASATA kwa ushirikiano walioutoa katika kuhakikisha wanatoa elimu kwa umma juu ya sanaa na uhamasishaji wa kushiriki uchaguziwa serikali za mitaa.
Mhe Magoti ameuambia umma kuwa sanaa ikitumika vizuri inageuka kuwa tiba ya mambo mengi yanayoonekana kuwa shida kwa wananchi kutokana na uwezo wake wa kuvuta hisia za jamii wanaosikia au kuona kazi ya sanaa husika, kingine wasanii wanaweza kujiajiri kupitia sanaa kutokana na mifumo iliyowekwa na kuendelea kuboreshwa na serikali ya awamu ya sita hivyo umefika muda muafaka kuchangamkia fursa hizo kwa kutoa kazi zenye ubunifu.

## Kutana na Jilema Ng'wana Shija mtaalam wa kuchalaza zeze


"Mnamo mwaka 1996 akiwa bado mtoto mdogo ndipo alipoanza kugundua kuwa ana mapenzi makubwa ya sanaa ya muziki hususani wa asili mara baada ya kumshuhudia baba yake akiwa analichalaza zeze katika matukio tofauti ya shughuli za kiutamaduni, kilimo na sherehe za kijamii ndani ya Kijiji cha Bukene wilayani Nzega, Mkoani Tabora ama kweli ile methali ya Mtoto wa nyoka ni nyoka imeakisi simulizi hii ya Gwiji wa Zeze"



Jilema Ng'wana Shija ni mwanamuziki aliyetimia kutokana na umahiri wake wa kutunga na uandishi wa mashairi yenye kukonga nyoyo za watu, kwa hakika amejaaliwa sana kuwa na uwezo wa kulichalaza zeze kiasi kwamba linamtii na kutoa sauti murua kwa namna anavyoliamuru zinazosindikizwa na mpangilio safi wa sauti zenye kuhamasisha uzalendo na furaha.

Utunzi na uwezo wake wa kuchalaza zeze umemuwezesha kumjengea ujasiri mkubwa wa kutoa tungo mbalimbali zilizokonga nyoyo za mashabiki wa muziki wa asili nchini kupitia nyimbo zake kama vile vijana na ukimwi, chapa ya ng'ombe, Sophia, igembe, selena, mele, niyele na wewe mwananchi ambapo mjumuiko wa nyimbo hizo zinaunda albamu yake aliyoitoa Novemba 4 mwaka 2018.

Anakiri kuwa kwa kipindi hicho wakati anatoa albam ya "Jilema Ng'wana Shija" hakufanikiwa kupata fedha zaidi ya umaarufu hivyo kumuwia vigumu sana kuendelea kumudu gharama ya kutoa albam nyingine ingawa uwezo bado anao, anaweza kufanya hayo yote kama tu akipata menejimenti nzuri yenye kuthamini maendeleo ya muziki wake.



Mkusanyiko huu wa nyimbo za asili zenye maudhui ya uhamasishaji katika ufanyaji kazi kwa bidi ni mfumo uliomjenga tangu akiwa mdogo na ameurithi kutoka kwa watamngulizi wake hususani Baba yake mzaizi ambaye alikuwa anamshuhudia akitumbuiza katika nyakati za msimu wa kulima na hata kipindi kile cha mavuno ambapo kwa maeneo ya kijijini kwao walitumia mtindo wa kushindana hivyo kuongeza hamasa kwenye uzalishaji.

Ng'wana Shija anaeleza kuwa, mwishoni mwa miaka ya 1980 alitumia muda mwingi kuambatana na Baba yake kila sehemu aliyoenda kutumbuiza kipindi cha msimu wa kilimo ndani ya Mkoa wa Geita, jambo hili lilisababish a kukosa muda wa kujiunga shule na kuhudhuria masomo ya darasani kwa wakati ule akili yake ilimuongoza na kumuaminisha kuwa ujuzi anaoupata ni elimu tosha itakayomsaidia katika Maisha yake hivyo akahamishia jitihada zote kwenye kucheza na zeze.

"Nakumbuka nikiwa mdogo kabisa mwanzoni mwa miaka ya 1980 nilikuwa naambatana sana na Baba yangu kila anapoenda kuimba na kwa kule kijijini hayakuwa matamasha makubwa isipokuwa ni yale ya kushindana na kuhamasisha kufanya kazi kwa bidi hususani wakati wa kulima kwa makundi au mavuno maarufu kwa jina la chapa ya ng'ombe kutokana na kufurahia hali hiyo sikupata nafasi ya kusoma" amesema Jilema.

Kuhama kwa wazazi wake kutoka Mkoa wa Geita kuelekea Wilaya ya Kaliua Mkoani Tabora miaka ya 2000 kulianza kumpa mwanga kwakuwa Baba yake alianza kumuamini na kumuachia asimamie kikundi chao cha muziki wa asili ambapo aliweza kufanya vizuri na kuibuka kidedea hasa kwenye mashindano ya kiutamaduni yaliyoshirikisha makundi mbalimbali ambayo yalihamasisha uzalishaji na uzalendo, umaarufu wake uliongezeka hadi akawa tishio kwa wengine kuogopa kuchuana nae.

Maisha yalianza kubadilika pale alipoamua kwa mara ya kwanza kufunga safari kutoka Mkoani Tabora na kuja jijini Dar es salaam ilikuwa mwaka 2007 ambapo alikuja kwa lengo moja tu kuendeleza muziki wa asili ambapo aliamini kanda ya ziwa ameshajitangaza vya kutosha kilichobaki ni kumfikia kila mtanzania na sehemu peke ya kufanikisha mkakati wake ni Dar es salaam.

Alipowasili jijini hakuapata changamoto sana kwakuwa alikuta wenyeji alioweza kushirikiana nao wakamuonesha njia na mbinu za upambanaji lakini kikwazo kikubwa kilikuwa ni udhaifu wake wa kutokujua kusoma wala kuandika, Maisha ya mjini yanaweza kuwa rahisi endapo kipaji kitaambatana na kujua kusoma na kuandika kwakuwa vitu havifanyiki kiholela hata kazi inapatikana kwa kusainiana mikataba hivyo ikamlazimu kuanza kujifunza kusoma na kuandika jambo ambalo halikumchukua muda mrefu.

Mara nyingi aliweza kupata kazi za kupiga katika maeneo mbalimbali ya starehe zikiwemo hoteli kubwa na kwenye kumbi za burudani hizo kazi zilimsaidia kwa kiasi kikubwa kuweza kuendesha Maisha yake ya hapa mjini hasa kupata mahitaji ya msingi, aliweza kufanya kazi zake kwa miaka 6 akarejea tena kwao Tabora kabla ya kurudi tena Dar es salaam mwaka mmoja baadae yaani 2014.

Jilema anaweka wazi kuwa mara baada ya kurejea mjini alianza kuona nyota imeanza kumuwakia kwani kazi zake zilianza kupata kibali cha mialiko ya kwenda kutumbuiza katika baadhi ya nchi za Afrika na Ulaya kwenye matamasha yenye hadhi ya kimataifa kutokana na mjumuiko wa washiriki wake kutoka maeneo mbalimbali Duniani ikiwemo Kenya 2016, Zambia 2017, Uturuki 2016, Denmark 2016, Ujerumani 2017, Norway 2019 zilimuwezesha kutanua wigo wa kufahamika kwa wadau mbalimbali ingawa hakuweza kuendelea kufanya nao kazi kutokana na kukosa menejimenti ya kumsimamia.

Pamoja na kipindi kirefu kuwa kimya huku akiendesha shughuli zake kupitia kutumbuiza katika Hoteli mbalimbali lakini sasa ameona umefika muda wa yeye kusimama tena kwakuwa serikali imeshaanza kutilia mkazo sekta ya sanaa hivyo ana matumaini makubwa kuwa kila jambo litaendelea kufanyika kiiutaalama ili kuboresha mnyororo wa thamani utakaomnufaisha kuanzia mzalishaji hadi msikilizaji wa maudhui ya kazi za sanaa.

Kutokana na hilo, ameiomba serikali kutilia mkazo mfumo wa elimu ya sanaa uwekwe katika somo kuanzia ngazi ya msingi ili kuwavuta wenye vipaji kama yeye wasikwepe kupata ujuzi huo kwa wakati, hapa, anaamini kwamba hata yeye wakati akiwa mdogo angeweza kuhudhuria masomo yake vizuri tu iwapo kungekuwa na elimu ya sanaa inayototolewa kikamilifu.

Sanaa sasa hivi ajira hivyo tunatakiwa kujivunia utamaduni wetu ili uwe kielelezo kwa watu wengine pale endapo sanaa yetu itafanikiwa kuvuka mipaka, ingawa katika hili kuna kasumba inayotawala hata miongoni mwa wasanii wenyewe kuwa matumizi ya ala za asili katika sanaa ni "ushamba" hii inatokana na usasa na kutothamini cha kwako jambo ambalo analipinga vikali Jilema Ng'wana Shija huku akimpa Kongole mwanamuziki mahiri Marioo ambaye alidiriki kumshirikisha kuweka "kionjo" katika wimbo wake wa "Hakuna Matata" ambao unaendelea kukimbiza sokoni.

Kwa sasa yupo katika hatua ya kutafuta wadau ambao wataweza kumsimamia kazi zake kulingana na mfumo wa soko la sasa kwakuwa bado ana utajiri mkubwa tungo zenye kusisimua, pia anakaribisha wasanii mbalimbali kushirikiana kwenye kazi kwakuwa utamduni ni kielelezo cha uzalendo, kujirasimisha ni msingi wa kuzikaribia fursa za sanaa zinazochagizwa na sera nzuri serikalini.



## “Hapa Awards” yawakutanisha kibiashara wasanii na wadau wa sanaa 133



Ule msemo wa “Sanaa ni ajira, biashara na uchumi” umedhihirika rasmi mara baada ya waanzilishi na waratibu wa tuzo za kimataifa zinazofahamika kama “Hollywood and African Prestigious Awards” (Hapa Awards) wakishirikiana na Baraza la Sanaa la Taifa na Bodi ya Filamu kufanikiwa kuwakutanisha wasanii na wadau wa sanaa zaidi ya 133 katika ukumbi wa Triniti Hotel uliopo Masaki jijini Dar es salaam tarehe 09 Agosti, 2024 kwa minajili ya kupeana mafunzo na fursa kabambe za kibiashara.
Mafunzo hayo yalilenga kuwapa ufahamu wa kutosha wasanii na wadau wa sanaa nchini juu ya kuboresha bidhaa yao ya kazi za sanaa ziwe na uwezo wa kuvutia mashabiki wa ndani na kimataifa pamoja na kuongeza wigo wa soko la bidhaa hizo bila kuhofia ushindani kutoka mataifa yaliyotangulia kimaendeleo katika tasnia ya sanaa.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo Makamu wa Raisi na mwanzilishi mwenza wa Hapa award Bi Amber Washington, amesema kuwa, amefurahi sana kuwepo Tanzania ingawa si mara ya kwanza ila safari hii imekuwa ya Faraja sana kwakuwa amepata kukutana na watu muhimu wa msingi ambao anahusiana nao moja kwa moja katika shughuli zake za kila siku ambao ni wasanii na wadau wa sanaa.
Ameendelea kusema kuwa Tanzania imebarikiwa sana kuwa na vipaji vingi katika tasnia ya kiwanda cha ubunifu “Creative industry” endapo vikiangaliwa kwa jicho la thamani vinaweza kuitoa hii nchi kutoka hatua moja kwenda nyingine kiuchumi ndiyo maana hawakusita walipopata mwaliko wa kuja Tanzania kwa ushawishi mkubwa wa BASATA na Bodi ya filamu wakishirikiana kwa ukaribu kabisa na Mama Mawini Kessy ingawa haikuwa kazi rahisi kushawishi wengine kuambatana lakini imekuwa hivyo.




Pamoja na mambo mengine Amber amesema kuwa mafunzo haya yatasaidia kubadilisha mitazamo ya watu wengi walio katika nchi zilizoendelea hususani Marekani wanakotoka wao ambapo kuna hali ya kutoamini sana wasanii wanaotoka nchi zinazoendelea, wanaamini sanaa ya Afrika ni duni haina ubunifu lakini leo hii wameambatana na baadhi ya wenzao ambao ndiyo mara ya kwanza kufika Afrika na kwa mshangao kabisa wamepigwa butwaa kuona kuna vitu vingi bora pengine kuliko Marekani hadi wanatamani watanzania namna wanaishi kwa umoja na amani, anaamini sanaa ni ubunifu na Maisha yanahitaji ubunifu.

Katika mafunzo hayo wadau mbalimbali walipata nafasi ya kutoa shuhuda za safari za mafanikio katika kiwanda cha sekta ya ubunifu kupitia muziki, uchoraji, mitindo, ujasiriamali, usimamizi wa wasanii, uendeshaji wa matukio, uongozi katika mashirikisho na vyama vya sanaa nchini.
Wote kwa pamoja wameshauriwa namna ya kuheshimu kazi zao, waweze kuuza bidhaa zao ambazo ni kazi za sanaa, waziweke katika mfumo wa ubunifu na ubora ambao utadumu kwa kipindi kirefu jambo ambalo litasaidia kujiuza zenyewe yaani maudhui yakitoka na kufanikiwa kuishi kwa walaji wao wanageuka kuwa mabalozi na wateja waaminifu kwao siku zote kikubwa wafahamu namna ya kuteka mioyo yao.

Chanzo chetu kimeongea na baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo ambapo kwa nyakati tofauti wamekiri kufurahishwa sana kufanyika kwa jukwaa hilo ambalo litakuwa daraja muhimu la kufikisha ujumbe wa yale mazuri yanayopatikana katika sanaa ya Tanzania pamoja na wageni wamekiri kutambua vipaji vilivyopo na kufurahia utamaduni unaoheshimika na kujali utu tofauti na mawazo yao hapo awali.




## Imechukua miaka 8 “hapa awards” kufanyika Afrika

Tarehe 10 Agosti, 2024 bara la Afrika limeweka historia ambapo kwa mara kwanza zimefanyika tuzo za “Hollywood and African Prestigious Awards” katika ukumbi wa Superdome uliopo Masaki, jijini Dar es salaam nchini Tanzania huku zaidi ya vipengele 43 vya tuzo vilitangaza washindi wake.

Vipengele hivyo vilihusisha 11 vya muziki, huku 21 vikiwa vya mitindo na vingine 11 vikihusisha tasnia ya filamu, taarifa imefafanua kuwa upande wa miziki iliyoshindaniwa imehusisha singeli, taarabu, dansi pamoja na ngoma za asili ambapo wasanii mbalimbali wamefanikiwa kuondoka na tuzo hizo.

Wasanii ambao wamenyakua tuzo mbalimbali katika usiku wa “hapa award” wamefanikiwa kuweka historia si tu hapa nchini bali kwa bara zima la Afrika kwakuwa tuzo hizi tangu kuanzishwa kwake zimekuwa zinafanyika huko Hollywood nchini Marekani ambapo zimefanyika kwa miaka saba mfululizo kabla yam waka huu kufanyika huu kufanyika nchini Tanzania.

Akiongea wakati wa utoaji wa tuzo hizo mgeni rasmi ambaye ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt Damas Ndumbaru amesema imekuwa furaha kwa tasnia ya sanaa kuendelea kufungua milango ya ushirikiano kimkakati hususani kimataifa hii itakuwa fursa ya kukuza ubora wa kazi na kufungua soko la kazi na kuongeza ubunifu kwa njia ya ushirikishwaji.

“Lengo la tuzo hizi ni kuendelea kuwajenga wasanii na wadau wa sanaa pamoja na kuwapa fursa ya kujulikana kimataifa, hivyo wasanii wa muziki, mitindo na filamu wanatakiwa kutumia fursa ipasavyo” amesema Dkt Ndumbaru.

Mhe Waziri ameweka wazi kuwa wasanii wa nchini wanatakiwa kufahamu kwamba serikali inafanya kazi kwaajili yao, mfano mzuri, tuzo hizo zimekuwa zikitolewa kwa miaka saba mfululizo huko Marekani lakini mwaka huu zimefanyika kwa mara ya kwanza nchini zikihusisha wasanii kutoka Marekani katika vipengele vya filamu bora, mwigizaji bora wa kike na wa kiume, wasanii bora wasaidizi, wachekeshaji bora na tamthiliya bora.

Ameendelea kusema kuwa huo ni mwanzo na matokeo chanya ya juhudi za serikali ya awamu ya sita kuhakikisha sekta ya sanaa inafungua kuwa chanzo cha ajira na kuwaingizia kipato cha uhakika kwa wadau wa sanaa pamoja na kutanua wigo wa ushirikiano kwa kuzingatia maadili na utamaduni wa Kitanzania kwakuwa anafahamu unavyoamua kukua kimataifa lazima uwe makini katika kuchangamana na tamaduni zisizoendana na utu.

Ameupongeza uongozi wa BASATA na Bodi ya filamu kwa kazi kubwa waliyoifanya wakishirikiana na Mama Mawini Kessy ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuunganisha pande mbili hadi kufanikisha kufanyika tukio hili la kihistoria kwa ukuaji wa tasnia ya sanaa nchini, ametoa ombi kwa waandaaji na waratibu wa tuzo hizo ikiwezekana zifanyike kwa mara nyingine nchini kwa ukubwa zaidi kwakuwa wizara iko tayari kutoa ushirikiano.

Katika kudhihirisha ukubwa wa tuzo hizo, nchi mbalimbali zimefanikiwa kushiriki katika tuzo hizo ni pamoja na Nigeria, Afrika ya kusini, Malawi, Zambia, Uganda, na Congo ambapo wote walifika katika ukumbi wa Superdome kushuhudia utoaji wa tuzo za kihistoria na kusherehekea thamani ya urithi wa utamaduni wa Kitanzania.

# Naibu katibu Mkuu Methusela Ntonda aipongeza BASATA



Naibu Katibu mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Bw. Methusela Stephen Ntonda ameipongeza Menejimenti ya baraza la sanaa la TAifa na kuwataka waongeze ubunifu katika utekelezzaji wa shughuli za kuenedleza sekta ya sanaa nchiniili kuongeza msukomo kwa wasanii katika kujiongezea kipato.

Ameyasema hayo tarehe 10 Agosti, 2024 wakati anaongea na timu ya wakuu wa idara na vitengo baada ya kutembelea ofisini hapo kwa minajili ya kujitambulisha na kutambua majukumu ya kuendeleza zsekta ya sanaa yaliyowasilishwa na Katibu Mtendaji Dkt. Kedmon Mapana katika taarifa ya utekelezaji.

Naibu Katibu mkuu ametanabaisha misingi ya utendaji wa kazi iambatane na ubunifu wa majukumu bila kuathiri taratibu huku lengo likiwa kukamilisha kwa mafanikio mikakati yote iliyopangwa katika taasisi kwa kipindi husika cha utekelezaji.
"Taasisi lazima iwe na mipango thabiti itakayokupa dira thabiti inayokuonesha umefika wapi na kama kuna mkwamo upo sehemu gani ili iwe arahisi kupata suluhisho, kwahiyo watumishi waongeze ubunifu ili kuweza kupiga hatua mbele zaidi" amesema Bw. Ntonda.

Alipogusiwa suala la changamoto ya mmomonyoko wa maadili katika sekta ya sanaa, Bw. Ntonda ameipongeza BASATA kwa kuwa na mwongozo wa uzingatiaji wa maadili katika shughuli za sanaa ambao umesambazwa kwa wadau wake, ila amesisitiza kuwa jambo hili ni mtambuka isiishie hapa washirikishwe na taasisi zingine ili na wao waweze kuwafikia jamii mzima.

"Suala la maadili linaendana na tabia ya mtu, watu na jamii kwa ujumla hivyo yapasa kuongeza nguvu katika ushirikishwaji ili kuwafikia taasisi zingine zisaidie kupaza sauti kwa jamii yote" ameongeza Ntonda.

Naibu Katibu Mkuu amefanya ziara hiyo ikiwa ni sehemu ya kutembelea na kujitambulisha kwa watumishi wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo mara baada ya kuteuliwa kushika nyadhifa hiyo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuapishwa Agosti mwaka huu.



# HERITAGE DRINKING WATER

Heritage Water – Okoa Pesa, Tunza Mazingira

HERITAGE
Drinking Water

Heritage Water – Okoa Pesa, Tunza Mazingira

## Jambo Tanzania!

Kampuni ya Heritage Drinking Water ilianzishwa April 7, 2020 ili kuisaidia serikali na jamii kupambana na uchafuzi wa mazingira utokanao na chupa tupu za maji na vimiminika vingine zilizozagaa mitaani. Kampuni ya Heritage inachakata na kuuza maji ya kunywa jijini Dar es Salaam.

Maji ya Heritage yana TDS ya 5 kwa mujibu wa vipimo vya shirika la viwango la Tanzania – TBS – kitu ambacho kinayafanya maji ya Heritage kuongoza kwa ubora Tanzania na wengine kujikongoja. Kwa takwimu za wateja, maji ya Heritage ni matamu yenye radha halisi ya maji. Heritage water hayawekewi kekimali yeyote ile na ni maji freshi kabisa – huchakatwa na kuuzwa siku/ saa/ dakika hiyo hiyo.

Maji ya Heritage hayapakiwi – hayafungwi moja kwa moja kwa seal – unakuja na chombo chako [kinakuwa sterilised] unaweka hela kwenye mashine, unabonyeza mashine kuchagua maji ya baridi au kawaida ili kukata kiu. Siku nyingine unarudi tena na chombo chako na utaratibu unakuwa huu huu na hivyo unakuwa huchafui mazingira. Bei za Heritage water ni za kitanzania – rejereja **lita 1 ni sh 250/=** na zaidi ya lita 60 lita 1 inakuwa **sh 200/=** hususani kwa deliveries za majumbani na maofisini.

Tunatoa huduma ya maji ya Heritage kwenye masherehe, michezo na matamasha.

heritagedrinkingwatertz@gmail.com

+255 656 000678; +255 687 838320

Heritage Water – Okoa Pesa, Tunza Mazingira

8 Barabara ya Kivukoni,
Utumishi, Kitalu C,
S. L. P 4779,
DAR ES SALAAM.

Simu: +255 738 259 611/481,
Baruapepe: km@basata.go.tz
info@basata.go.tz

Mfumo wa Wadau wa Sanaa,
Jisajili kupitia: https://sanaa.go.tz

**www.basata.go.tz**

**basata.tanzania**